**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

Kumb.Na.MCC/J.10/1/VOL.V/50 31, Julai, 2023

# TANGAZO KWA UMMA(MARUDIO)

Ofisi ya MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA inawatangazia wananchi wote kwamba Halmashauri ya Jiji la Mbeya linakusudia kutunga na kufanya marekebisho ya Sheria Ndogo zifuatazo:

1. **SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) MAREKEBISHO, ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2023**
2. **SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) MAREKEBISHO, ZA HALMASHAURLA MBEYA ZA MWAKA 2023.**
3. **SHERIA NDOGO ZA (USIMAMIZI WA MASOKO) MAREKEBISHO, ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2023.**
4. **SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) MAREKEBISHO, ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2023.**
5. **SHERIA NDOGO ZA (USIMAMIZI WA MAHUDHURIO,LISHE NA CHAKULA CHA WANAFUNZI SHULENI), 2023 (UTUNGAJI)**

Endapo kuna mtu yeyote ana pingamizi au maoni kuhusu mapendekezo ya kufanya marekebisho ya Sheria Ndogo zilizotajwa hapo juu basi awasilishe ndani ya kipindi cha wiki mbili kuanzia tarehe ya tangazo hili lililotolewa leo tarehe 31/07/2023.
TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO TAREHE 31.07.2023 NA

Davis L. Mbembela
K.n.y MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JJI
**MBEYA**

**Nakala:** **Vyombo vya habari na tovuti ya Halmashauri ya Jiji**

**Mbao zote za Matangazo**

**Stendi na Masoko yote.**

**TANGAZO LA SERIKALI Na.................. la Tarehe........................**

## SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
## (SURA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1)*

## SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2023

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Hifadhi ya mazingira) (Marekebisho) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2023, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka, 2020 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Marekebisho GN Na. 836 ya tarehe 2/10/2020

2. Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu Katika kifungu cha 6 (4) kwa kuongeza maneno yafuatayo baada ya neno Mahakama *"fedha zitakazopatikana zitafidia gharama za utunzaji wa mfugo/mifugo pamoja na faini na kiwango kitakachobaki kitarudishwa kwa mwenye mifugo"*

**TANGAZO LA SERIKALI Na.................. la Tarehe........................**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**
**(SURA 290)**

---

**SHERIA NDOGO**

---

***(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1)***

**SHERIA NDOGO ZA (USIMAMIZI WA MASOKO) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2023**

| | | |
|---|---|---|
| Jina na tarehe ya kuanza kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Usimamizi wa Masoko) (Marekebisho) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2023, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Usimamizi wa Masoko) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka, 2020 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| Marekebisho GN Na. 838 ya tarehe 2/10/2020 | 2. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu Katika kifungu cha 3 sehemu ya tafsiri ya neno Mkurugenzi kwa kuongeza maneno yafuatayo baada ya neno Mbeya “ *pamoja na Afisa yoyote atakayeteuliwa kutekeleza Majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi”*. |

**TANGAZO LA SERIKALI Na.................. la Tarehe.........................**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**
**(SURA 290)**

**SHERIA NDOGO**

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2023**

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) (Marekebisho) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2023, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka, 2020 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Marekebisho GN Na. 909 ya tarehe 16/10/2020

Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu nakuongeza Jedwali la 19 na kuandika kama ifuatavyo;

**19. USHURU WA KUPAKIA NA KUSHUSHA MIZIGO**

| NA. | UZITO WA GARI | KIASI ( kwa kila tripu) |
|---|---|---|
| 1. | Tani 1-3 | 3,000 |
| 2. | Tani 4-7 | 5,000 |
| 3. | Tani 8-11 | 10,000 |
| 4. | Tani 11-14 | 15,000 |
| 5. | Tani 15-30 | 20,000 |
| 6. | Tani zaidi ya 30 | 25,000 |

**TANGAZO LA SERIKALI Na.................. la Tarehe.........................**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**
**(SURA 290)**

---

**SHERIA NDOGO**

---

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2023**

| | | |
|---|---|---|
| Jina na tarehe ya kuanza kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) (Marekebisho) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2023, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka, 2020 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| Marekebisho GN Na. 909 ya tarehe 16/10/2020 | 2. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu Katika Jedwali la 13 Na. 1 kwa kufuta maneno *"uimbaji kwenye tamasha Tshs. 100,000/="* na kuandika kama ifuatavyo; |

1. Uimbaji kwenye Matamasha

    (i) Waimbaji wakubwa Tshs. 100,000/=

    (ii) Waimbaji wadogo Tshs. 50,000/=

**TANGAZO LA SERIKALI Na.................. la Tarehe........................**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**
**(SURA 288)**

---

**SHERIA NDOGO**

---

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)*

**SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2023**

| | | |
|---|---|---|
| Jina na tarehe ya kuanza Kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Afya na usafi wa mazingira) (Marekebisho) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2023, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Afya na usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka, 2020 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 2. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu Katika kifungu cha 3 kuondoa neno choo cha kuvuta na iandikwe choo cha maji. |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 3. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu Katika kifungu cha 3 kwa kuondoa maana ya choo bora iliyopo na kuandikwa "*maana yake ni choo chenye sakafu inayosafishika kwa maji, kuta imara za kudumu zilizo kamilika, kiwe na paa lililoezekwa mlango, na sehemu ya kunawia mikono kwa maji tiririka na sabuni baada ya kutoka chooni.* |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 4. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu Katika kifungu cha 3 kwa kuondoa maana ya neno uchunguzi wa afya nakuongeza maneno yafuatayo "*Maana yake ni kupima afya yake katika vituo vya afya vinavyomilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini iwapo kuna vimelea vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi, kasha kupewa cheti cha uthibitisho wa upimaji huo."* |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 5. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu Katika kifungu cha 8 kwa kuondoa neno |

"*Halmashauri itafanya uhamasishaji*" na kuongeza maneno yafuatayo "*itakuwa ni jukumu la.*"

| | | |
|---|---|---|
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 6. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria Ndogo kuu katika kifungu cha 11 kwa kuongeza kifungu kidogo cha 4 na kitasomeka "*Ni marufuku kwa mtu yeyote au barabara kwa shughuli zozote bila kibali toka Halmashauri ya Jiji la Mbeya.*" |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 7. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 13 kwa kuondoa neno Bwana Afya na kuandika Afisa Afya. |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 8. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 14 kwa kuondoa neno "mbao safi" na kuandika neno "aluminium." |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 9. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 14 kwa kuondoa neno "mbao safi" na kuandika neno "aluminium." |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 10. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 15 kwa kuondoa neno "kuuza vyakula visivyopikwa vimewekwa chini" na kuandika neno "kuuza bidhaa za chakula kwa kutandaza ama kupanga chini." |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 11. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 18 (1) (a)-(f) kwa kuondoa maneno; |

(a) ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu,

(b) lina maji safi, magogo na misumeno ya kukatia nyama;

(c) lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na sehemu za mizani;
(d) lina pipa la kuhifadhia taka taka;.
(e) muuzaji ana vazi jeupe pamoja na aproni nyeupe;
(f) muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita.

na kuandika maneno;

(a) ni jengo la kudumu lenye ukubwa usiopungua futi 10 kwa futi 10 kwa futi 12, na sakafu ya marumaru nyeupe lina maji safi, magogo na misumeno ya kukatia nyama;
(b) lina maji safi, magogo na misumeno ya kukatia nyama na kuta za ndani ziwe na marumaru nyeupe.
(c) liwe na mlango wa vioo, jokofu la kuhifadhi nyama na meza ya saruji yenye marumaru nyeupe.
(d) lina pipa la kuhifadhia taka taka;.
(e) Muuzaji avae koti safi jeupe, apron, kofia na viatu vyeupe.
(f) muuzaji anapima afya yake kabla na kila baada ya miezi sita katika vituo vya afya vilivyopo chini ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya na kupatiwa cheti.

Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020

12. Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 20 kwa kuondoa maneno "anapata kibali kutoka Halmashauri kabla hajaanza biashara" na kuandika neno "Jengo lake linafanyiwa ukaguzi wa kiafya na kupata idhini ya kuanza biashara baada ya kukidhi kanuni za kiafya."

Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020

13. Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 22 (1) kwa kuondoa maneno "Itakuwa ni wajibu wa kila Mmiliki wa hoteli, wafanyakazi wa machinjio, mgahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari kupima afya kila baada ya miezi sita na watalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu tano (Tsh.5,000/=).
" na kuandika maneno "Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa biashara ya chakula, viwanda vya

| | | |
|---|---|---|
| | | vyakula, hoteli migahawa, machinjio,bucha, kuoka mikate, nyumba za kulala wageni, baa, grosari, samaki wabichi na wakavu, maziwa na bidhaa zozote za vyakula, kuhakikisha wahudumu/wafanyakazi kwenye biashara hizo wanapimwa afya zao kabla na kila baada ya miezi sita katika vituo vya afya vya Jiji na watalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu kumi (Tsh.10,000/=)." |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 14. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 22 (2) kwa kuondoa maneno "*Mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza atalazimika kupima afya kila baada ya miezi sitana atalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha* kiasi cha shilingi elfu tano (Tsh.5,000/=).<br>na kuandika maneno *"Mtu yeyote anayetengeneza ama kuandaa chakula kwa ajili ya kuuza ama kutoa huduma atalazimika kupima afya yake kabla na baada ya miezi sita na atalipa ada ya shilingi elfu kumi (Tshs 10,000).*" |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 15. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 22 (3) kwa kuongeza maneno "*na kutovaa sare kamili"* na kusomeka<br>*"Mmiliki yeyote atakayeruhusu mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake na kutovaa sare kamili atakuwa ametenda kosa."* |
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 16. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 25 kwa kuondoa maneno "*Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara ambayo viwango vyake vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza laSheria Ndogo hizi.*"<br>na kuandika maneno *"Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa kiafya wa jengo ambayo italipwa kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara kwa maombi mapya na maombi ya marudio (re newal) ambayo viwango vyake vitakuwa kama vilivyo ainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi"* |

| | | |
|---|---|---|
| Marekebisho GN Na.837 ya Tarehe 2/10/2020 | 17. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 26 (1) kwa kuondoa maneno *"Ada ya ukaguzi wa afya italipwa kila mwanzo wa mwaka wa fedha wa Halmashauri yaani mwezi Julai."* na kuandika maneno "*Ada ya ukaguzi wa kiafya wa jengo italipwa kila mwanzo wa maombi mapya ya biashara yoyote na wakati wa marudio ya leseni."* |
| | 18. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 40 kwa kuondoa maneno "Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote." na kuandika maneno " Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo bora na safi kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote ." |
| | 19. | Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 40 kwa kuondoa maneno "Itakuwa ni wajibu wa mtu, kikundi, Taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa madhumuni ya ujenzi, sherehe au sehemu yoyote ambayo itakutanisha watu kwa muda maalum endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri." na kuandika maneno "*Itakuwa ni wajibu wa mtu, kikundi, Taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa madhumuni ya mkutano, ujenzi, kongamano, tamasha, sherehe au sehemu yoyote ambayo itakutanisha watu kwa muda maalum endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri."* |

20. Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 44 kwa kuondoa maneno *"Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo viwili vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hizi kwa ajili ya matumizi ya wateja wake wa jinsia zote."*

na kuandika maneno

*""Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo viwili vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hizi kwa ajili ya matumizi ya wateja wake wa jinsia zote na watu wenye mahitaji maalum."*

21. Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika kifungu cha 50 kwa kuongeza kifungu vidogo (l), (m), (n), (o), (p) and (q) na kuweka maneno:

(l). Ataweka nguo na viatu kwenye bucha

(m). Atachanganya vyakula vilivyopikwa na vibichi kwenye jokofu moja.

(n). Atasafirisha nyama kwenye mfuko wa sandarusi.

(o). Atauza chakula chochote bila kuvaa sare kamili.

(p). Atafanya maziko ya maiti ya binadamu au kiumbe chochote kwenye eneo la makazi, biashara au taasisi.

(q). Kuhamia na kuishi kwenye nyumba isiyokuwa na choo.

22. Marekebisho yamefanyika katika Sheria ndogo kuu katika Jedwali la kwanza kwa kuondoa neno *"Ada ya ukaguzi wa Afya"* na kuandika neno "*Ada ya ukaguzi wa kiafya katika Jengo*".

TANGAZO LA SERIKALI NA…....la tarehe …………..

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**(SURA YA 288)**

---

**SHERIA NDOGO**
**(Zimetungwa chini ya Kifungu na 89)**

**Sheria Ndogo za (Usimamizi wa Mahudhurio, Lishe na Chakula cha wanafunzi shuleni) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2023.**

| | | |
|---|---|---|
| **Jina na tarehe ya kuanza kutumika** | **1.** | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Usimamizi wa mahudhurio, lishe na chakula cha wanafunzi shuleni) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2023 na zitaanza kutumika kuanzia tarehe kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| **Eneo la Matumizi** | **2** | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya ya Jiji la Mbeya. |
| **Tafsiri ya maneno** | **3** | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itahitajika vinginevyo; |

**"Chakula"** maana yake ni chakula cha mchana kinachotolewa shuleni.

**"Halmashauri"** maana yake ni Halmashauri ya ya Jiji la Mbeya

**Lishe.** Maana yake ni hali inayotokana na kula Mlo kamili na wakutosha wenye mchanganyiko wa vyakula vya makundi matano ikiambatana na mazoezi ya mwili ambayo ni msingi wa afya njema.

"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya ya Jiji la Mbeya pamoja na afisa ye yote wa Umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

**"Shule"** maana yake ni shule za msingi na sekondari zilizomo ndani ya eneo la Halmashauri ya ya Jiji la Mbeya;

**"Mzazi"** maana yake ni baba au mama au mlezi wa mtoto aliyeandikishwa Shule;

**"Mlezi"** maana yake ni mtu yeyote aliyekabidhiwa kumlea mtoto aliyeandikishwa Shule;

**"Mwanafunzi"** ni mtu au mtoto yeyote anayesoma katika shule ya msingi au sekondari katika Halmashauri ya ya Jiji la Mbeya.

**"Serikali ya Mtaa"** maana yake ni Serikali ya Mtaa, Kamati ya maendeleo ya Kata na Halmashauri ambayo shule hiyo ya msingi au Sekondari ipo.

**"Sheria"** maana yake ni Sheria Ndogo za (usimamizi wa lishe, mahudhurio na chakula shuleni) za Halmashauri ya Halmashauri ya ya Jiji la Mbeya za mwaka 2023.

"**Umri wa kwenda Shule**" maana yake ni umri kati ya miaka mitano mpaka sita (5-6) kwa elimu ya awali miaka sita hadi saba (6-7) kwa darasa la kwanza na Sekondari ni umri baada ya kumaliza darasa la saba.

**Kuandikishwa na mahudhurio**

**4.** **(1)** Itakuwa ni wajibu wa lazima kwa kila mzazi au mlezi kumuandikisha na kusimamia mahudhurio ya mtoto wake shuleni na kufuatilia maendeleo yake kwa kushirikiana na waalimu wa shule husika.

**Uundaji wa timu ya Kata ya usimamizi wa michango ya chakula shuleni.**

**5.** **(1).** Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila Mtaa au Kata itaunda timu ya wajumbe wasiozidi watano ambao kati yao wajumbe wasiopungua wawili lazima wawe wanawake. Kwa ajili ya kusimamia na kuratibu upatikanaji wa chakula na michango ya chakula shuleni, na katibu wa timu hiyo atateuliwa miongoni mwa walimu katika shule husika au mwalimu anayehusika na masuala ya chakula na lishe katika shule husika.

**(2).** Timu ya usimamizi na uratibu wa chakula iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) katika sheria ndogo hizi itadumu kwa muda wa miaka 3 na itakuwa na majukumu ya;

(i) Kufuatilia na kusimamia matumizi ya fedha zote za chakula shuleni ili ziweze kuleta tija na ziendane na matumizi husika.

(ii) Kukusanya na Kuhimiza michango yote inayotolewa na walezi/wazazi kama ilivyo elekezwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(iii) Kushirikiana na wazazi/walezi katika jamii kuweka utaratibu wa chakula kwa wanafunzi wa kutwa na hosteli.

(iv) Kusimamia na kuratibu usimamizi na upatikanaji wa chakula shuleni.

(v) Kuandaa mazingira/sehemu nzuri kwa ajili ya utoaji wa chakula kwa wanafunzi shuleni.

(vi) Kusimamia na kuwasaidia watoto watokao katika kaya masikini zenye wazazi wasio na uwezo, wenye mazingira magumu na hatarishi pamoja na yatima wasiojiweza kupata chakula shuleni.

**(3).** Timu iliyoundwa na Mtaa itawajibika kwa kamati ya shule au bodi ya shule na serikali ya Mtaa na timu iliyoundwa na kata itawajibika kwa kamati ya maendeleo ya kata.

**Wajibu/majukumu ya Halmashauri**

**6.** **(1)** Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi Halmashauri itakuwa na majukumu yafuatayo;

(i). Kuandaa na kusimamia utekelezaji wake kwa ufanisi mipango na bajeti kila mwaka inayo zingatia mahitaji halisi ya Elimu msingi bila malipo na lishe na afua za lishe, bila kusahau mahitaji ya wanafunzi na walimu. Mipango na bajeti hizi zihusishe pia watoto wote wenye rika lengwa waliopo katika vituo shikizi, na elimu nje ya mfumo Rasmi katika ngazi hiyo;

(ii) Kuratibu utoaji mipango na bajeti za ruzuku ya uendeshaji wa shule ikiwemo ulinzi, umeme, maji, na ununuzi wa chaki na karatasi pamoja na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia;

(iii) Kuandaa takwimu sahihi za wanafunzi wote zikiainisha wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kila shule vikiwemo vitengo na shule zisizo za Serikali

(iv) Kutenga na kutumia fedha shuleni kwa wakati kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa mitihani na majaribio mbalimbali shuleni ikiwemo tathmini endelevu.

(v) Kutenga na kutumia fedha shuleni za kununua samani yakiwemo madawati, vifaa vya michezo, matengenezo ya mashine na mitandao pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya shule;

(vi) Kutenga fedha za Ruzuku ya uendeshaji wa shule; asilimia 60% elimu ya msingi na asilimia 50% elimu ya sekondari kwa

ajili ya kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa elimu maalum.

(vii) Kutenga na kutumia fedha shuleni za kugharamia chakula wanafunzi wa kutwa na wa bweni, nauli wakati wa kwenda na kurudi likizo pamoja na vifaa na visaidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum waliopo kwenye shule na vitengo vya elimu maalum;

(viii) Kutenga na kutumia fedha shuleni za usimamizi na utoaji wa elimu ya watu wazima kwa kugharamia vifaa vya kufundishia na kujifunza pamoja na malipo kwa walimu wanaofundisha madarasa husika.

(ix) Kutenga na kutumia fedha shuleni kwaajili ya watoto walioko kwenye mazingira hatarishi,yatima na wengine wa aina hiyo kulingana na miongozo ya serikali kuhusu maswala haya;

(x) Kusambaza miongozo ya Elimu msingi bila Malipo na kukagua matumizi sahihi ya fedha na Ruzuku za uendeshaji na uendelezaji wa shule.

(xi) Kuendelea kutoa elimu kwa umma na kuhakikisha jamii katika kujitolea nguvu kazi na mali ili kuleta ustawi na maendeleo ya shule zilizopo ndani ya jamii husika;

(xii) Kutathmini mazingira ya shule za kutwa na kumshauri katibu Tawala Mkoa kuhusu kutoa kibali cha huduma za chakula cha mchana au huduma ya chakula kwa wanafunzi wa hosteli kwa shule za Halmashauri.

(xiii) Kutenga fedha za kugharamia uendeshaji wa mitihani ya ndani na kitaifa kulingana na idadi ya wanafunzi walio katika shule za serikali;

(xiv) Kuweka mipango na bajeti kwa ajili ya kutoa motisha kwa walimu na wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo vipaji na vipawa;

(xv) Kutoa elimu ya kilimo na ufugaji shuleni.

(xvi) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhusiana na ubora na usalama wa chakula shuleni.

**Wajibu/Jukumu la wakuu wa shule.**

7. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Walimu wakuu wa shule ya msingi na wakuu wa shule za sekondari watafanya yafuatayo;

(i) Kusimamia shughuli zote za taaluma, utawala na uendeshaji wa shule.

(ii) Kuwapa maelekezo wazazi kuhusu aina ya vifaa vinvyohitajika mfano rangi ya kitambaa cha sare ya shule, sare za michezo, idadi na aina ya madaftari wakayotumia wanafunzi ili wazazi waweze kununua wenyewe.

(iii) Kusimamia na kuhakikisha kwamba fedha inayotolewa na serikali inatumika kama ilivyo kusudiwa kulingana na taratibu za miongozo ya fedha za serikali;

(iv) Kutoa takwimu na taarifa sahihi za idadi ya wanafunzi na mahitaji mengine ya shule;

(v) Kuanzisha jukwaa la wazazi na walimu ili kujadiliana masuala mbalimbali ya Elimu msingi bila malipo;

(vi) Kushirikiana na jamii kuweka utaratibu wa kutoa huduma ya chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa au kutoa chakula na huduma nyingine kwa wanafunzi wa hosteli na kupeleka maombi kwa katibu Tawala wa Mkoa kupitia kwa Mkurungezi wa Halmashuri ya ya Jiji la Mbeya;

(vii) Kushirikiana na walimu katika kubaini changamoto zitokanazo na mpango wa utekelezaji wa Elimu Bila Malipo na kuwasilisha mapendekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri;

(Viii) Kutenga chumba maalum na safi kwa ajili ya kuhifadhi chakula cha wanafunzi shuleni.

(ix) Kuandikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule bila masharti au malipo yoyote.

(x) Kugawa fomu kwa wanafunzi waliofaulu kujiunga na shule iliyotolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Wajibu na majukumu ya kamati/bodi za shule.** | **8.** | **(1)** | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kamati na Bodi za shule za serikali kama kiungo muhimu cha wazazi na walezi na shule, zitakuwa na wajibu kusimamia vyema uendeshaji wa shule kwa kufanya yafuatayo;<br><br>(i) Kufuatilia na kusimamia matumizi ya fedha zote za shule ili ziweze kuleta tija;<br><br>(ii) Kuhakikisha kuwa sera,nyaraka,maelezo na miongozo ya serikali inazingatiwa na kutoa ushauri stahiki;<br><br>(iii) Kushirikisha jamii katika maazimio ya masuala mbalimbali yanayohusu maslahi na maendeleo ya shule kwa ujumla kama vile ulinzi na upatikanaji wa walimu wa muda au wa mkataba, kwa masomo ya Sayansi, Hisabati na Ufundi.<br><br>(iv) Kuwasilisha maazimio yanayohusu uchangiaji wa hiari kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa lengo la kupata kibali;<br><br>(v) Kushirikiana na wazazi/ jamii kuweka utaratibu wa chakula cha mchana au chakula cha huduma za hosteli katika shule za kutwa kulingana na mazingira yao na kuwasilisha mapendekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. |
| **Wajibu na majukumu ya walimu** | **9.** | | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Walimu wanawajibu wa kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora kulingana na mazingira yaliyopo kwa kuahakikisha anatekeleza yafuatayo;<br><br>(i) Anazingatia sera na nyaraka, maelekezo na miongozo ya serikali kuhusu utoaji Elimumsingi bila Malipo<br><br>(ii) Anatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kazi yake ikiwemo kutoa mrejesho kwa mzazi au mlezi kuhusiana na maendeleo ya mtoto wake.<br><br>(iii) Anawaongoza na kuwasaidia wanafunzi kupata elimu bora na kukua katika maadili mema ili waweze kuwa raia wema watakaoshiriki kikamilifu katika maendeleo yao, familia, jamii na taifa kwa ujumla<br><br>(iv) Anakuwa na maadili mema na utendaji uliotukuka siku zote ili awe mfano wa kuigwa na wanafunzi wake na<br><br>(v) Anatoa ushauri nasaha na unasihi kwa watoto wenye matatizo mbalimbali ya kijamii na kitaaluma. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Wajibu na majukumu ya wanafunzi** | **10** | **(1)** | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi Wanafunzi wa Elimu msingi na sekondari katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya au yeyote atayehamia katika shule za msingi au sekondari zilizopo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya watawajibika kutekeleza majukumu yafuatayo;<br><br>(i) Kwenda shule na kuhudhuria masomo kulingana na ratiba ya shule na kalenda ya shule.<br><br>(ii) Kuwa na maadili mema wakati wote hivyo kuacha kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa kanuni mbalimbali za shule, maadili na sheria za nchi.<br><br>(iii) Kutoa mrejesho kwa mzazi au mlezi kuhusu alichojifunza ili wafahamu na kuweza kumsaidia ipasavyo katika masomo yake.<br><br>(iv) Kutoa mrejesho kwa mzazi au mlezi kuhusu jambo lolote linaloagizwa shuleni ili mzazi au mlezi ashiriki kikamilifu katika maendeleo ya shule |
| **Wajibu /Majukumu ya viongozi na jamii katika mamlaka za mitaa.** | **11.** | **(1)** | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi viongozi wa serikali za Mitaa na kata, dini na jamii katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya watahakikisha wanatekeleza wajibu na majukumu yafuatayo;<br>(i) Kuhamasisha wazazi au walezi wenye watoto wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa shuleni.<br><br>(ii) Kufuatilia na kutoa ushirikiano kwa shule na wazazi au walezi katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wanakuwa shuleni wakati wa masomo badala ya kuzurura mitaani au kuwa kwenye shughuli ambazo hazihusiani na masomo.<br><br>(iii) Kutoa ushirikiano katika shughuli zote za kuleta maendeleo ya kielimu katika maeneo yao ili kuweza kupata matokeo tarajiwa kwa wakati na;<br><br>(iv) Kuendelea kujitolea nguvukazi na mali ili kuleta ustawi na maendeleo ya shule zilizoko ndani ya jamii.<br><br>(v) Kuhakikisha wanatoa elimu na kuhamasisha umuhimu wa wazazi kutoa chakula kwa wanafunzi shuleni. |

(vi). Kusimamia na kuelimisha watoto elimu ya maadili na nidhamu katika jamii kwa kukemea tabia mbaya na matendo mabaya katika jamii.

**Wajibu/Jukumu la mzazi au mlezi.** **12** **(1)** Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kila mzazi au mlezi Atahakikisha kuwa mtoto wake mwenye umri wa kwenda shule anapelekwa shuleni na anahudhuria masomo mpaka atakapomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari kidato cha kwanza mpaka cha nne.

**(2)** Mzazi au mlezi wa mwanafunzi atakuwa na wajibu wa;

(a). Kuhakikisha kwamba kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule anandikishwa katika shule.

(b). Kuhakikisha kwamba kila mtoto aliyefaulu kujiunga na kidato cha kwanza anasajiliwa na kuendelea na masomo.

(c). Anawajibu wa kusimamia na kufuatilia mahudhurio ya mtoto shuleni.

(d). Anatoa mchango wa chakula uliowekwa na Serikali ya Mtaa au Kamati ya maendeleo ya kata.

(e). Anamnunulia vifaa vya shule na mavazi ya shule.

(f). Anafuatilia mwenendo na tabia ya mtoto.

(g). Kulipa nauli ya kwenda na kurudi kwa wanafunzi wa kutwa, na hosteli wakati wa likizo;

(h). Kukemea na kutoa taarifa kwa ngazi husika kuhusu mienendo inayokwenda kinyume na Elimu msingi Bila Malipo.

**Utaratibu na mfumo wa** **13** **(1)** Kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki kila Mzazi au Mlezi atawajibika kuchangia debe mbili za mahindi, nusu debe la maharage au fedha sawa na bei ya sokoni pamoja na

| | | | |
|---|---|---|---|
| **mchango wa chakula** | | | mchango wa Tshs.4,000/= au kiasi kitakachopangwa na mamlaka husika kwa kila mwanafunzi kwa Mwaka kama mchango wa chakula cha mchana na gharama za mpishi. |
| | | **(2)** | (i) Uchangiaji wa moja kwa moja kwa njia ya fedha au misaada kwa ajili ya Mpango wa chakula shuleni.<br><br>(ii) Kushiriki katika utekelezaji wa mpango wa uchangiaji chakula kwa watoto ambao wazazi wao au walezi hawana uwezo wa kuchangia ambao wamethibitishwa na uongozi wa Mtaa na Shule. |
| | | **(3)** | Fedha zitapokelewa na Kamati ya chakula na kutunzwa kwenye akaunti. |
| **Makosa na Adhabu kwa mzazi au mlezi chini ya sheria ndogo hii.** | **14** | **(1).** | Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria hii, kwa mzazi au mlezi kutokujali au kukataa kuchangia mchango wa chakula cha mchana ikiwa; |
| | | **(a)** | Atadharau, au atakaidi kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na Mpango wa uchangiaji wa chakula cha mchana shuleni kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi; |

**(b).** Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kushiriki kutekeleza Mpango wa uchangiaji chakula cha mchana shuleni;

**(c)** Atatoa kwa makusudi huku akijua ni kosa taarifa za uongo kwa Halmashauri;

**(d)** Atashindwa kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

**(e)** Atamzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake.

**(f)** Atasababisha au kumzuia kwa makusudi mtoto mwenye umri wa kuanza shule kumsajili shuleni au anayesoma kumzuia au kusababisha mwanafunzi kushindwa kuhudhuria masomo kwa mujibu wa kalenda ya shule;

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua laki mbili 200,000/= au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) jela au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo.

**Makosa ya jinai na adhabu kwa mujibu wa sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 toleo la 2022.**

**15** **(1)** Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya mapenzi, kumchumbia, kuoa au kuoza, au kumpa mimba mwanafunzi au mtoto wa umri chini ya miaka 18 au mwanafunzi aliyehitimu akisubiri matokeo atachukiliwa hatua kali za kisheria kwa mujibu wa sheria ya Kanuni za adhabu ikiwa ni pamoja na kumpeleka polisi na kumfungulia kesi mahakamani kwa mujibu wa sheria za nchi.

**(2)** Ni marufuku kwa mzazi au mlezi kumuozesha mwanafunzi kwa ridhaa yake au anasubiri matokeo kabla ya matokeo kutangazwa au kutoroka kwa nia ya kuolewa au kuoa na akipatikana na hatia hiyo atakuwa ametenda kosa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria kwa mujibu wa sheria za nchi.

**Kufifilisha kosa**

**16..** Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi Laki mbili (200,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa

maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi isipokuwa kwa makosa yaliyoanishwa katika kifungu cha 15 yatashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za haki jinai zilizotungwa na Bunge.

Nembo na Mhuri wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya imebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe ………………………..

Mbele ya

***Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya***

***Halmashauri ya Jiji la Mbeya***

***Mstahiki Meya***

***Halmashauri ya Jiji la Mbeya***

**NAKUBALI**

**Dodoma,** ANGELA KAIRUKI., **(Mb)**

**Tarehe……../………../………** ***Waziri wa Nchi- OR- TAMISEMI***